**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**634** **STADI ZA KAZI**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2018**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali **kumi na sita (16).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila Sehemu **B** na **C**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Taja njia nne zinazotumika kuhifadhia picha na mapambo mbalimbali katika somo la Stadi za Kazi.
2. (a) Fasili dhana ya majigambo.
   (b) Fafanua kwa ufupi faida mbili za majigambo katika jamii.
3. Baini faida nne za uvaaji wa nguo kwa binadamu.
4. Eleza kwa kifupi njia nne zinazoweza kutumika kufundishia mada ya Upishi kwa wanafunzi wa Darasa la Tano.
5. Taja mambo manne yanayofanya kuwepo kwa usawa wa kijinsia katika ufundishaji.
6. Fafanua manufaa manne ya ubunifu katika ufundishaji.
7. Eleza maana ya istilahi mwafaka, ridhimu, kilele na kigao kama zinavyotumika kwenye fani ya Muziki.
8. Bainisha faida nne za kutumia mbinu ya majadiliano katika kufundisha mada ya Biashara Ndogondogo.
9. Onesha umuhimu wa Urazini wa Ujumi katika maisha ya kila siku.
10. Bainisha makundi manne ya mboga kwa kutoa mifano.

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **Mawili** katika sehemu hii.

11. Eleza sababu tano za kuweka urembo kwenye nguo na bidhaa nyingine.
12. Fafanua faida sita za kupika chakula kwa njia ya kuchemsha.
13. Chambua faida sita za Ususi.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **Mawili** katika sehemu hii.

14. Fafanua hasara sita zinazoweza kujitokeza kwa kufundisha mada ya Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo bila kutumia zana za kufundishia na kujifunzia.
15. (a) Chambua mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini.
    (b) Eleza faida tatu za kutayarisha jedwali la utahini katika upimaji.
16. Chambua vigezo sita ambavyo mwalimu anapaswa kuzingatia katika kuchagua mbinu za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org